# Wasira asema hakuna chama kilicho juu ya sheria

**NA MWANDISHI WETU**

**MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wasira, amewahakikishia Watanzania kwamba Chama hakina chuki wala kısası na mtu yeyote na kinaamini sera ya maridhiano.**

Aidha alisema hakuna chama chochote cha siasa kilicho juu ya sheria na kwamba kinapofanya kosa lolote kitakumbana na mkono wa sheria.

Wasira alitoa kauli hiyo jana katika mkutano wa hadhara alipokuwa akizungumza na wana CCM na wananchi wa Wilaya ya Urambo mkoani Tabora ambako ni muendelezo wa ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani, kuzungumza na viongozi wa CCM na kusikiliza kero za wananchi.

Aidha alisema CCM inaamini maridhiano ni sera ya Chama na serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na ndio maana hata Tundu Lissu alipokuwa amekimbia nchi maridhiano ndiyo yalimrudisha nchini.

"Jamani mkiwa na sera ya maridhiano haiwi mbadala wa sheria na wala huwezi kusema kwani sote tuko chini ya sheria hata mimi nikiamka sasa hivi nikakupiga kofi Jeshi la Polisi watanikamata hawawezi kusema wewe ni Makamu Mwenyekiti wa CCM maana umakamu haunipi uhuru wa kupiga watu makofi halafu nikaondoka salama", alisema Wasira.

Alitumia fursa hiyo kuwataka chama cha CHADEMA kufuata sheria zilizopo ili kuona kwamba hakuna mvutano baina yao na vyombo vya sheria.

"Unapoamini kuwa sisi ni chama cha maridhiano na wewe unataka uridhiane na sisi tunakubali una hoja yako, labda tuwaachie wenye kushtaki waelewane kule mahakamani halafu mambo yao yakiisha sisi tutakaa naye na tutazungumza",

alisema Wasira.

Awali Shabani Swae Mushio Warioba, ambae ni mwanachama wa CHADEMA alitoa ombi kwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Wasira, akidai amemsikia Mwenyekiti wa chama chake cha CHADEMA yuko ndani, hivyo anataka kujua amefanya kosa gani na kama amefanya kosa anaiomba serikali ya Chama Cha Mapinduzi imsamehe hata kama ana makosa.




***MSAJILI wa Hazina Zanzibar, Waheed Mohammad Ibrahim Sanya (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari huko ofisini kwake Maisara, juu ya uzinduzi wa tuzo za umahiri katika mawasiliano Zanzibar. Tunzo hizo zitatolewa kwa ushirikiano na taasisi ya Uhusiano wa Umma Tanzania (IPRT) na Idara ya Habari Maelezo Zanzibar. (PICHA NA ABDALLA OMAR).***

# Vijana watakiwa kushirikiana na ZAECA kuzuia rushwa

**NA ASYA HASSAN**

**VIJANA nchini wametakiwa kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) katika juhudi za kuzuia na kudhibiti vitendo vya rushwa vinavyoweza kujitokeza katika nyanja mbalimbali za maisha, hususan wakati wa uchaguzi mkuu.**

Wito huu umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA, Ali Abdalla Ali, wakati wa mkutano maalum ulioandaliwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na viongozi wa Mabaraza ya Vijana Zanzibar, hafla ambayo ilifanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakili Kikwajuni Mjini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kuwa rushwa haipati nafasi ya kuathiri maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa nchini.

"Hatua hizi si tu zitaimarisha demokrasia pia zitasaidia kujenga taifa lenye misingi imara ya haki na usawa, vijana wanapochukua jukumu hili, wanathibitisha kuwa wao ni nguzo muhimu katika kujenga mustakabali bora wa taifa," alisema.

Aidha alifahamisha kuwa rushwa imekuwa kikwazo kikubwa katika mchakato wa uchaguzi ikisababisha kupotea kwa haki za wapiga kura na kuathiri matokeo ya uchaguzi, endapo vijana watakuwa na nguvu na ari ya mabadiliko basi wana nafasi ya kuleta mabadiliko chanya.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa wakati umefika sasa kwa vijana kushiriki kikamilifu katika kampeni za kuelimisha umma, kufichua vitendo vya rushwa na kuhimiza uwazi katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Alibainisha kuwa vijana ni nguzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya kijamii, hivyo ni muhimu kujiepusha kutumiwa vibaya na wanasiasa kwa kushiriki katika vitendo vya rushwa, kwani rushwa inaharibu maadili ya jamii na kukwamisha maendeleo ya taifa.

"Mchango wa vijana ni msingi imara katika kujenga jamii yenye maadili na uwajibikaji, hivyo ushirikiano Wenu ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa rushwa inatokomezwa kabisa hapa nchini," alisema.

Aidha alitumia fursa hiyo kuwataka vijana kuwa mabalozi wa kuelimisha wenzao kuhusu madhara ya rushwa na kuhimiza uwazi jambo ambalo litasaidia kufanyika kwa uchaguzi wa haki na bila kuathiriwa na vitendo vya rushwa.

Nae Katibu Mtendaji Baraza la Vijana Zanzibar, Ali Haji Hassan, alisema katika kuelekea uchaguzi mkuu baraza hilo limekuja na kampeni maalum ya kuhamasisha vijana na suala la amani inayojulikana kwa jina la 'Amani ni tunu, vijana tuienzi'.

Alisema kupitia kampeni hiyo itasaidia vijana kuendeleza amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi ili kuhakikisha taifa linaendelea kuwa na utulivu na amani, hali ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu.

Akizungumzia mafunzo hayo aliishukuru ZAECA kwa kuwapatia mafunzo hayo kwani rushwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya jamii na kusema kuwa vijana wana nafasi ya kipekee ya kuleta mabadiliko hayo.

Kwa upande wake Mwanasheria kutoka Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) Maulid Ame Mohammed akiwasilisha mada ya wajibu wa vijana kuzuia rushwa katika uchaguzi mkuu alisema uchaguzi unamchakato mkubwa ambao ndani yake unaweza unaweza kuwa na viashiria vya rushwa.

"Vijana mna haki ya kushiri katika uchaguzi hivyo ni vyema kuitumia vizuri haki yenu ya kidemokrasia bila ya kujiingiza katika vitendo hivyo kwani vitaweza kuwaathiri", alisema.

Akiwasilisha mada ya wajibu wa vijana katika kuzuia rushwa katika uchaguzi mkuu, Ofisa Elimu kutoka ZAECA, Yussuf Juma Suleiman, alisisitiza umuhimu wa vijana kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha uwazi na uadilifu katika mchakato wa uchaguzi.

Alisema uchaguzi ukitawaliwa na rushwa utasababisha athari mbalimbali, hivyo vijana wanawajibu wa kuchukua hatua ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika kwa uwazi, haki na uadilifu.

# ZARI kuchunguza mbegu za mazao kuepuka maradhi

**NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM**

**TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) imesema itaendelea kushirikiana na wakulima wa mazao mbali mbali ili kuzifanyia uchunguzi mbegu za mazao mbali mbali ili kuepukana na maradhi yanayoathiri uzalishaji mashambani.**

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Mohamed Dhamir Kombo, alieleza hayo aliposhiriki zoezi la uvunaji wa muhogo katika shamba la utafiti wa mbegu liliopo Kizimbani, wilaya ya Magharibi 'A', Unguja.

Alisema utafiti huo umetoa aina nane mpya za mbegu ya zao la muhogo zinazostahamili maradhi ya michirizi ya kahawia na batobato hivyo wataendelea kushirikiana na wakulima ili kuijua mbegu nzuri na itakayoleta matokeo mazuri kwao.

Hata hivyo alisema baada ya uchunguzi wa mbegu hizo wataanza kuzisambaza katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ili wakulima waweze kufaidika nazo.

Mapema Mkuu wa Divisheni ya Utafiti wa Udongo na Afya ya Mimea, Ali Hamad Ali, amesema lengo la jaribio hilo ni kutafuta mbegu yenye kustahamili maradhi ya michirizi, kahawia na batobato

Alisema kupitia mbegu hizo wataona uwezo wake na ustahamilivu wa maradhi na kuahidi kuendelea kuzisambaza kwa wakulima wengine katika mashamba tofauti baada ya taasisi ya utafiti wa kilimo kuthibitisha ubora wa mbegu hizo.

Alieleza kuwa baada ya kuvuna na kupima uzalishaji wa mbegu hizo itasaidia kuibua na kutambua kiwango cha upatikanaji wa muhogo kwa hekta za ulimaji.

Naye mmoja ya wakulima walioshiriki zoezi hilo kutoka mkoa wa Kaskazini Unguja, Ali Haji Bakari, alieleza kufarijika kwake kushirikishwa katika utafiti wa uchaguzi wa mbegu, jambo litakalowashajihisha kuendelea kulima kwa kutumia mbegu bora na kutumia njia za kisasa.

Aliongeza kuwa kufanya hivyo kutanyanyua uzalishaji wa zao hilo na mengine hivyo kuongeza faida kwa mkulima mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Utafiti huo umefanywa katika kituo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa uhimilivu wa mifumo ya chakula Tanzania unaotekelezwa tanzania bara na Zanzibar chini ya wizara zinazohusika na kilimo.

PDF Scanner ACE Scanner